

## KISWAHILI

### UMAHIRI WA KUSIKILIZA PESNO VII YA KWANZA 2021

Mgeni wa ajabu alipozuru eneo lao alipenda mandhari tulivu ya mahali pale. Wenyeji walidhani mgeni atawadhuru watoto wao, wakaacha kuzurura na kurandaranda ovyo. Watu wazima hawakumuelewa vizuri, wakatafuta udhaifu wa yule mgeni. **Walitumia mizania** ya kila namna ili apate kudhihirisha udhaifu wa madhara yake.

Siku moja, mtu mmoja nadhifu aliyevalia mavazi maridhawa, alifanya dharura na kuanza kuzurura ili tu aone huyo mgeni wa ajabu kama atadhihirisha tabia ya kudhuru watu. Siku hiyo, haikutokea hata ishara moja ya kuashiria kuwa alitaka kumdhuru.

Baada ya siku kadhaa kupita, ilidhihirika kuwa katika maeneo yote aliyozuru mgeni yule, hakumdhuru mtu yeyote. Watoto walianza kumdhihaki. Watu wazima waliwadhibiti watoto wasiendeleo kumdhihaki.